**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Pakistan**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Jumanne, 14 Dhu al-Hijjah 1441 H** **04/08/2020 M** **Na: 1441 / 85**

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## Kutia Chumvi Vidonda Vyetu na Kuyatusi Majeshi Yetu, Serikali ya Bajwa-Imran Yatoa Wimbo katika Kumbukumbu ya Kwanza ya Uunganishwaji kwa Nguvu wa Kashmir Iliyo Kaliwa

Kwa mnasaba wa kumbukumbu ya kwanza ya uunganishwaji kwa nguvu wa Kashmir iliyo kaliwa na Muungano wa India, 5 Agosti 2020, serikali ya Bajwa-Imran imetoa wimbo kupitia ISPR, ikiiomba India kuondoka Kashmir Iliyo Kaliwa na kuchochea shutma zilizo enea kwa Waislamu wa Pakistan. Je, historia ishawahi kushuhudia kurudi nyuma kwa dhalimu yeyote mvamizi kupitia maombi, achilia mbali wimbo?! Moto, damu na chuma pekee ndio hulazimisha kurudi nyuma kwa madhalimu wavamizi, kama ilivyo tokea katika ukombozi wa Kashmir iliyo kombolewa (Azad), kupitia Jihad. Baada ya kusubiria kwa mwaka mzima kuhamasishwa kwa majeshi yaliyo tayari ya Pakistan, Waislamu wa Kashmiri Iliyo Kaliwa, na Pakistan badala yake wameshuhudia serikali ikiimba na miito mitupu. Hakika, serikali imetia chumvi vidonda vyetu na kuyatusi majeshi yetu, kwa kujionyesha kwa Modi kuwa mashini zetu za vita hazina uwezo na kwamba serikali imelazimika kugeukia sekta ya burudani.

Vipi tutaiamini serikali ya Bajwa-Imran kuhifadhi yoyote katika maslahi na matukufu yetu, wakati ambapo wale ambao wanaweza kufanya biashara na mishipa yetu ya damu, wanaweza kuuza mwili mzima? Licha ya kuziamuru ndege za kivita za kisasa, vifaru, makombora ya masafa marefu, nyambizi, manuari, mifumo ya ulinzi ya angani, mizinga mikubwa, silaha za kimbinu na kistratejia za kinyuklia za kisasa, na zaidi ya simba laki sita walio na hamu ya ushindi au shahada, serikali dhaifu ya Bajwa-Imran imegeukia uimbaji, upigaji picha katika Mpaka wa Udhibiti na kuipa jina upya barabara. Kwa kufanya hivyo serikali hii ya khiyana imeipa idhini Dola ya Kibaniani kusherehekea kumbukumbu hii na kuendelea kujimakinisha, bila ya changamoto yoyote.

**Enyi Waislamu katika Majeshi ya Pakistan!** Serikali ya Bajwa-Imran imefichua khiyana yake, kwa kuwazuia kurahisisha uvamizi wa Dola ya Kibaniani, kwa maagizo ya Amerika. Sauti ambazo ndugu zetu na dada zetu katika Kashmir Iliyo Kaliwa wanazitamani, ni mingurumo ya ndege za kivita na vifaru vyenu, milipuko ya mizinga na makombora yenu na radi ya kutetemesha ya nyayo zenu na takbira.

Mtume wa Mwenyezi (saw) amesema,

«مَنْ لَمْ يَغْزُ أَوْ يُجَهِّزْ غَازِيًا أَوْ يَخْلُفْ غَازِيًا فِي أَهْلِهِ بِخَيْرٍ أَصَابَهُ اللَّهُ بِقَارِعَةٍ»

**"Yeyote ambaye hajapigana (Jihad) au kumuandaa mpiganaji au kuisaidia kwa kheri familia ya mpiganaji, Mwenyezi Mungu atamsibu kwa msiba ugongao kabla ya Siku ya Kufufuliwa"** (Abu Dawood). Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

«وَاعْلَمُوا أَنَّ الْجَنَّةَ تَحْتَ ظِلَالِ السُّيُوفِ»

**"Na jueni kwamba Pepo iko chini ya vivuli vya panga"** (Abu Dawood). Sio demokrasia wala udikteta utakao waruhusu kufuata amri ya Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw) ya kutekeleza Jihad, ili kupata utukufu wa duniani na cheo cha juu Akhera. Imetosha sasa, hivyo basi

sitisheni uhaini njiani mwake. Toeni Nusra mara moja kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah kwa Njia ya Utume. Hapo na hapo pekee ndipo mtakapo ongozwa na Khalifah Muongofu katika kuikomboa Kashmir Iliyo Kaliwa, ili mnyanyue bendera ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) eneo la Srinagar, katika siku ambayo washirikina wa Kibaniani watachukia na Waumini watafurahi.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Pakistan**

**Tovuti:** www.hizb-pakistan.com http://HizbPK.page.tl
**Pepe:** HTmediaPAK@gmail.com **WhatsApp: +90-531-814-7385**
**Twitter**: http://Twitter.com/HTmediaPAK **Facebook:** https://Facebook.com/HTmediaPAK10
**YouTube**: http://YouTube.com/HTmediaPAK **Dailymotion:** https://Dailymotion.com/HTmediaPAK
**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info